# SENSA YA UZALISHAJI VIWANDANI 2013

## MUHTASARI WA RIPOTI

## TANZANIA BARA



***Dira***
*Kuwa kitovu cha takwimu rasmi nchini.*

***Dhamira***
*Kutoa takwimu rasmi zilizo bora na huduma zinazokidhi mahitaji ya wadau wa kitaifa na kimataifa kwa ajili ya kupanga mipango na kutoa maamuzi.*

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Kwa taarifa zaidi kuhusiana na Muhtasari wa Ripoti ya Sensa ya Uzalishaji Viwandani, 2013 zinapatikana:

Ofisi ya Taifa ya Takwimu,
18 Barabara ya Kivukoni,
S.L.P. 796,
11992 Dar es Salaam – Tanzania.

Simu: +255 22 2122722/3 | Nukushi: +255 22 2130852 | Anuani ya barua pepe: dg@nbs.go.tz |
Tovuti: www.nbs.go.tz

**Nukuu inayoshauriwa ni:**

Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji (MITI), Sensa ya Uzalishaji Viwandani, 2013: *Muhtasari wa Ripoti*. Dar es Salaam.

**Ofisi ya Taifa ya Takwimu**
**Wizara ya Fedha na Mipango**

**Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji**

**Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania**

**Machi, 2016**

# YALIYOMO

**Orodha ya Majedwali** ........ **iv**

**Orodha ya Michoro** ........ **iv**

**1.0 Utangulizi** ........ **1**

**2.0 Aina ya Viwanda** ........ **2**

2.1 Idadi ya Viwanda Katika Sekta Ndogo za Viwanda ........ 2

2.2 Idadi ya Viwanda kwa Shughuli za Uzalishaji Viwandani ........ 4

2.3 Idadi ya Viwanda Ki-Mkoa ........ 6

2.4 Idadi ya Viwanda katika Makundi ya Wafanyakazi ........ 8

2.5 Idadi ya Viwanda Kulingana na Aina ya Umiliki ........ 11

2.6 Idadi ya Viwanda kwa Msingi wa Umiliki Kisheria ........ 11

**3.0 Idadi ya Wafanyakazi Viwandani** ........ **13**

3.1 Idadi ya Wafanyakazi Katika Sekta Ndogo za Viwanda ........ 13

3.2 Idadi ya Wafanyakazi Kijinsia Katika Sekta Ndogo za Viwanda ........ 13

3.3 Idadi ya Wafanyakazi kwa Shughuli za Viwanda ........ 14

3.4 Idadi ya Wafanyakazi Ki-Mkoa ........ 16

3.5 Idadi ya Wafanyakazi Katika Sekta Ndogo za Viwanda ........ 17

**4.0 Malipo kwa Wafanyakazi** ........ **18**

4.1 Malipo kwa Wafanyakazi Katika Sekta Ndogo za Viwanda ........ 18

**5.0 Ongezeko la Thamani** ........ **19**

5.1 Ongezeko la Thamani katika Sekta Ndogo za Viwanda ........ 19

5.2 Ongezeko la Thamani Katika Shughuli za Viwanda ........ 20

5.3 Ongezeko la Thamani Ki-Mkoa ........ 22

## Orodha ya Majedwali

Jedwali Na. 1: Idadi ya Viwanda Katika Shughuli za Uzalishaji Viwandani, Tanzania Bara, CIP 2013 ..... 5
Jedwali Na. 2: Idadi ya Viwanda katika Sekta Ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani Ki-Mkoa na Makundi ya Wafanyakazi, Tanzania Bara, CIP 2013 ..... 8
Jedwali Na. 3: Idadi ya Viwanda vya Utengenezaji wa Bidhaa kwa shughuli ya Kiwanda na Ukubwa wa Ajira, Tanzania Bara, CIP 2013 ..... 10
Jedwali Na. 4: Idadi ya Viwanda Kulingana na Aina ya Umiliki ..... 11
Jedwali Na. 5: Idadi ya Viwanda kwa Msingi wa Umiliki Kisheria na Ukubwa wa Ajira, Tanzania Bara, CIP 2013 ..... 12
Jedwali Na. 6: Idadi ya Wafanyakazi kwa Sekta Ndogo za Viwanda na Ukubwa wa Ajira, Tanzania Bara, CIP 2013 ..... 13
Jedwali Na. 7: Idadi ya Wafanyakazi Kijinsi kwa Sekta Ndogo za Viwanda na Ukubwa wa Ajira, Tanzania Bara, CIP 2013 ..... 14
Jedwali Na. 8: Idadi ya Wafanyakazi kwa Shughuli za Viwanda, Tanzania Bara, CIP 2013 ..... 15
Jedwali Na. 9: Malipo kwa Wafanyakazi Katika Sekta Ndogo za Viwanda na Ukubwa wa Ajira, Tanzania Bara, CIP 2013 ..... 18
Jedwali Na. 10: Ongezeko la Thamani kwa Sekta Ndogo za Viwanda na ukubwa wa Ajira, Tanzania Bara, CIP 2013 ..... 19
Jedwali Na. 11: Ongezeko la Thamani kwa Shughuli za Viwanda na Ukubwa wa Ajira, Tanzania Bara, CIP 2013 ..... 20
Jedwali Na. 12: Ongezeko la Thamani kwa Sekta Ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani, Tanzania Bara, CIP 2013 ..... 21
Jedwali Na. 13: Mgawanyo wa Ongezeko la Thamani Katika Viwanda vya Utengenezaji Bidhaa Viwandani kwa Makundi ya Wafanyakazi, Tanzania Bara, CIP 2013 ..... 21
Jedwali Na. 14: Ongezeko la Thamani katika Secta Ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani, Tanzania Bara, CIP 2013 ..... 22
Jedwali Na. 15: Ongezeko la Thamani kwa Mkoa na Ukubwa wa Ajira, Tanzania Bara, CIP 2013 ..... 23

## Orodha ya Michoro

Mchoro Na. 1: Idadi ya Viwanda Vyote katika Sekta Ndogo za Viwanda, Tanzania Bara, CIP 2013 ..... 3
Mchoro Na. 2: Idadi ya Viwanda Vikubwa Vyenye Wafanyakazi Kumi au Zaidi katika Sekta Ndogo za Viwanda, Tanzania Bara, CIP 2013 ..... 3
Mchoro Na. 3: Idadi ya Viwanda Vidogo Vyenye Mfanyakazi Mmoja Hadi Wafanyakazi ..... 4
Mchoro Na. 4: Idadi ya Viwanda Vikubwa Vyenye Wafanyakazi Kumi au Zaidi Ki-Mkoa, Tanzania Bara, CIP 2013 ..... 6
Mchoro Na. 5: Idadi ya Viwanda Vikubwa Vyenye Wafanyakazi Kumi au Zaidi katika Sekta Ndogo ya Uzalishaji wa Bidhaa Viwandani Ki-Mkoa, Tanzania Bara, CIP 2013 ..... 7
Mchoro Na. 6: Idadi ya Viwanda kwa Makundi ya Wafanyakazi, Tanzania Bara, CIP 2013 ..... 9
Mchoro Na. 7: Idadi ya Wafanyakazi Ki-Mkoa, Tanzania Bara, CIP 2013 ..... 16
Mchoro Na. 8: Asilimia ya Wafanyakazi kwa Makundi ya Wafanyakazi, Tanzania Bara, CIP 2013 ..... 17

# 1.0 UTANGULIZI

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji (MITI), na Shirikisho la wenye Viwanda Tanzania (CTI) ilifanya Sensa ya Uzalishaji Viwandani ya mwaka 2013. Kihistoria Sensa ya Viwanda ni ya Nne kufanyika Tanzania Bara tangu kupatikana kwa uhuru mwaka 1961. Kwa mara ya kwanza Sensa ya Viwanda ilifanyika mwaka 1963 ikifuatiwa na mwaka 1978 na 1989.

Sensa ya Uzalishaji Viwandani imefanyika kwa msaada wa kiufundi uliotolewa na shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO) na fedha zilitolewa na Serikali ya Tanzania na Washirika wa Maendeleo kupitia fungu linalotolewa kwa ajili ya Mpango Kabambe wa Kitaifa wa Kuboresha na Kuimarisha Takwimu Tanzania (Tanzania Statistical Master Plan - TSMP).

Lengo kuu la Sensa ya Uzalishaji Viwandani lilikuwa ni kutoa taarifa sahihi zinazohusu sekta ya viwanda na ambazo zitatumika katika kutathmini mchango wa sekta ya viwanda kwa uchumi wa Nchi. Aidha, sensa ilikuwa na lengo la kutoa taarifa za msingi ambazo zitatumika kufanikisha tafiti nyingine na kuwezesha uchambuzi wa mipango mbalimbali, utungaji wa sera na kusaidia katika kufanya maamuzi sahihi.

Sensa ya Uzalishaji Viwandani ya mwaka 2013 imehusisha viwanda vyote vyenye maeneo ya kudumu Tanzania Bara kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Mgawanyo wa Shughuli za Uzalishaji na Utoaji Huduma (ISIC) toleo Namba 4 ili kuhakikisha ulinganishi kimataifa. Sensa hii imejumuisha viwanda vyote vilivyojishughulisha na Uchimbaji madini na mawe; Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani; Uzalishaji na usambazaji wa Umeme, gesi, mvuke na kubadilisha hali (joto/baridi); na Kukusanya, kutibu na kusambaza maji. Hata hivyo, sekta ndogo ya utengenezaji wa bidhaa viwandani ndiyo inayoongoza katika sekta zote ndogo za uzalishaji viwandani. Kwa hiyo, mwelekeo wa ukuaji wa sekta nzima ya viwanda kwa kiasi kikubwa, ulitegemea uzalishaji wa sekta hii ndogo.

Utengenezaji wa bidhaa viwandani unahusu ubadilishaji wa malighafi kuwa bidhaa mpya kwa kubadilisha muundo na maumbo. Bidhaa zinazobadilishwa ni malighafi ambazo zinatokana na kilimo, misitu, uvuvi, uchimbaji madini na mawe pamoja na bidhaa za shughuli nyingine za utengenezaji wa bidhaa viwandani ambazo ni malighafi kwa sekta hii. Shughuli za ubadilishaji, urekebishaji wa bidhaa pia hutambulika kama utengenezaji wa bidhaa viwandani.

Madhumuni ya ripoti hii ni kuwasilisha kwa muhtasari, matokeo muhimu yanayohusu Sensa ya Uzalishaji Viwandani ili kutoa rejea muhimu juu ya nini kinapatikana kwenye ripoti kuu. Ripoti imetoa kwa ufupi, matokeo muhimu yanayohusu aina na mifumo mbalimbali ya viwanda husika, ajira na malipo yake, pato ghafi, gharama za uzalishaji na ongezeko la thamani. Matokeo haya yamegawanyika kulingana na aina ya uzalishaji, ukubwa wa kiwanda kulingana na idadi ya wafanyakazi, eneo la kijiografia mahali kiwanda kilipo na hali ya umiliki.

# 2.0 AINA YA VIWANDA

## 2.1 Idadi ya Viwanda Katika Sekta Ndogo za Viwanda


Ili kukidhi mahitaji ya Sera ya Nchi kuhusu Viwanda Vidogo na vya Kati (SMEs), viwanda viligawanywa katika makundi makuu mawili kama ifuatavyo:

1. **Viwanda vikubwa**; vyenye idadi ya wafanyakazi kumi au zaidi (10+). Idadi yake ilikuwa 1,322 sawa na asilimia 2.7 ya viwanda vyote kwa mwaka 2013. Kundi hili liligawanywa katika makundi madogo matano; viwanda vyenye wafanyakazi 10 hadi19, 20 hadi 49, 50 hadi 99, 100 hadi 499, na wafanyakazi 500 au zaidi.

2. **Viwanda vidogo**; vyenye idadi ya mfanyakazi mmoja hadi wafanyakazi tisa. Idadi ya viwanda hivi ilikuwa 47,921 sawa na asilimia 97.3 ya viwanda vyote kwa mwaka 2013. Kundi hili liligawanywa katika makundi madogo mawili; wafanyakazi wasiozidi wanne na lile lenye wafanyakazi kuanzia watano hadi tisa.


Matokeo yanaonesha kuwa, katika jumla ya viwanda vyote 49,243 **(vikubwa na vidogo)** vilivyohusika katika Sensa ya Uzalishaji Viwandani kwa mwaka 2013, sekta ndogo ya utengenezaji wa bidhaa viwandani iliongoza kuwa na idadi kubwa ya viwanda 48,474 (asilimia 98.4) kuliko sekta yoyote ndogo, ikifuatiwa na uchimbaji madini na mawe 391 (asilimia 0.8); usambazaji maji, usimamizi wa maji taka, uthibiti wa taka na shughuli za kutibu maji 227 (asilimia 0.5); na ya mwisho ilikuwa uzalishaji na usambazaji wa umeme, gesi, mvuke na kubadilisha hali (joto/baridi) yenye viwanda 151 sawa na asilimia 0.3 ya viwanda vyote.

**Mchoro Na. 1: Idadi ya Viwanda Vyote Katika Sekta Ndogo za Viwanda, Tanzania Bara, CIP 2013**





Kuhusu viwanda vikubwa, matokeo yanaonesha kuwa; kati ya viwanda 1,322, sekta ndogo ya utengenezaji wa bidhaa viwandani ilikuwa na viwanda 998 sawa na asilimia 75.5 ya viwanda vyote vya sekta hii, ikifuatiwa na sekta ndogo ya uchimbaji madini na mawe viwanda 210 (asilimia 15.9), kukusanya, kutibu na kusambaza maji viwanda 87 (asilimia 6.6) na ya mwisho ilikuwa uzalishaji na usambazaji wa umeme, gesi, mvuke na kubadilisha hali (joto/baridi) ambayo ilikuwa na viwanda 27 au asilimia 2.0 ya viwanda vyote vikubwa.

**Mchoro Na. 2: Idadi ya Viwanda Vikubwa Vyenye Wafanyakazi Kumi au Zaidi Katika Sekta Ndogo za Viwanda, Tanzania Bara, CIP 2013**



Kwa upande wa viwanda vidogo vyenye mfanyakazi mmoja hadi wafanyakazi tisa, matokeo yanaonesha kuwa, katika jumla ya viwanda 47,921, utengenezaji wa bidhaa viwandani ulikuwa na viwanda 47,475 sawa na asilimia 99.1 ya viwanda vyote vya sekta hii ndogo, ikifuatiwa na sekta ndogo ya uchimbaji madini na mawe viwanda 182 (asilimia 0.4), usambazaji maji, usimamizi wa maji taka, uthibiti wa taka na shughuli za kutibu maji viwanda 140 (asilimia 0.3) na ya mwisho ilikuwa uzalishaji na usambazaji wa umeme, gesi, mvuke na kubadilisha hali (joto/baridi) ambayo ilikuwa na viwanda 124 sawa na asilimia 0.3 ya viwanda vyote vidogo.

**Mchoro Na. 3: Idadi ya Viwanda Vidogo Vyenye Mfanyakazi Mmoja Hadi Wafanyakazi Tisa Katika Sekta Ndogo za Viwanda, Tanzania Bara, CIP 2013**




## 2.2 Idadi ya Viwanda kwa Shughuli za Uzalishaji Viwandani

Idadi ya viwanda kwa kila shughuli ya uzalishaji hutofautiana kutoka shughuli moja hadi nyingine. Shughuli nne za uzalishaji zilizoongoza zimechangia asilimia 52.8 ya jumla ya idadi ya viwanda, nazo ni: utengenezaji wa bidhaa za chakula viwanda 19,696 (asilimia 40.0); utengenezaji wa bidhaa za nguo 13,392 (asilimia 27.2); utengenezaji wa samani 6,823 (asilimia 13.9); na utengenezaji wa bidhaa za chuma isipokuwa mitambo na vifaa viwanda ilikuwa na viwanda 3,805 (asilimia 7.7).


**Jedwali Na. 1: Idadi ya Viwanda Katika Shughuli za Uzalishaji Viwandani, Tanzania Bara, CIP 2013**

| Shughuli ya Kiwanda | Idadi ya Viwanda | Asilimia |
|---|---|---|
| Utengenezaji wa bidhaa za chakula | 19,696 | 40.0 |
| Utengenezaji wa mavazi | 13,292 | 27.0 |
| Utengenezaji wa samani | 6,823 | 13.9 |
| Utengenezaji wa bidhaa za metali, isipokuwa mitambo na vifaa | 3,805 | 7.7 |
| Utengenezaji wa mbao na bidhaa zitokanazo na mbao, fomaika, isipokuwa samani; utengenezaji wa bidhaa zinazotokana na mabua na malighafi za kusukia | 1,770 | 3.6 |
| Utengenezaji wa bidhaa zingine za madini zisizo za metali | 1,103 | 2.2 |
| Utengenezaji wa nguo | 708 | 1.4 |
| Uchimbaji wa madini mengine na mawe | 347 | 0.7 |
| Utengenezaji wa vifaa vya umeme | 253 | 0.5 |
| Kukusanya, kutibu na kusambaza maji | 222 | 0.4 |
| Utengenezaji wa ngozi na bidhaa zinazohusiana | 177 | 0.4 |
| Utengenezaji mwingine wa bidhaa vya viwandani | 175 | 0.4 |
| Upigaji chapa na uandaaji wa media zilizonakiliwa | 168 | 0.3 |
| Uzalishaji na usambazaji wa umeme, gesi, mvuke na kubadilisha hali(joto/baridi) | 151 | 0.3 |
| Utengenezaji wa mashine/mitambo na vifaa ambavyo havijatajwa | 99 | 0.2 |
| Utengenezaji kemikali na bidhaa za kemikali | 88 | 0.2 |
| Utengenezaji wa vinywaji | 76 | 0.2 |
| Utengenezaji wa bidhaa za mpira na plastiki | 65 | 0.1 |
| Utengenezaji wa vyombo vingine vya usafiri | 47 | 0.1 |
| Uchimbaji wa metali ghafi | 44 | 0.1 |
| Utengenezaji wa magari na matela ya malori | 37 | 0.1 |
| Ukarabati na ufungaji wa mitambo na vifaa | 28 | 0.1 |
| Utengenezaji wa metali za msingi | 19 | 0.0 |
| Utengenezaji wa karatasi na bidhaa za karatasi | 18 | 0.0 |
| Utengenezaji wa bidhaa za tumbaku | 14 | 0.0 |
| Utengenezaji wa madawa ya binadamu, kemikali za kutibia na bidhaa za mimea | 7 | 0.0 |
| Ukusanyaji taka, shughuli za kutibu na kutupa taka; urejeshaji nyenzo | 5 | 0.0 |
| Utengenezaji wa makaa ya mawe na bidhaa za mafuta ya petroli iliyosafishwa | 3 | 0.0 |
| Utengenezaji wa kompyuta, vifaa vya kielektroniki na uoni | 2 | 0.0 |
| Uchimbaji wa Makaa ya mawe magumu na mepesi | 1 | 0.0 |
| **Jumla** | **49,243** | **100.0** |

## 2.3 Idadi ya Viwanda Ki-Mkoa

Idadi ya viwanda kimkoa kwa viwanda vikubwa vyenye wafanyakazi kumi au zaidi, matokeo yanaonesha kuwa; kutoka jumla ya viwanda 1,322, Mkoa wa Dar es Salaam uliongoza kwa kuwa na viwanda 389 (asilimia 29.4%) , ukifuatiwa na mikoa ya Manyara 167 (asilimia 12.6); Arusha 89 (asilimia 6.7) na Kilimanjaro viwanda 66 (asilimia 5.0). Hata hivyo, kwa mkoa wa Manyara, viwanda 149 sawa na asilimia 89.2 ya viwanda vinavyoshiriki katika shughuli za uchimbaji wa madini vilihusika zaidi na uchimbaji madini ya tanzanite.


**Mchoro Na. 4: Idadi ya Viwanda Vikubwa Vyenye Wafanyakazi Kumi au Zaidi Ki-Mkoa, Tanzania Bara, CIP 2013**




*Viwanda vingi vilihusika na uchimbaji wa madini ya tanzanite

Kwa upande wa sekta ndogo ya utengenezaji wa bidhaa viwandani, matokeo yanaonesha kuwa, katika jumla ya viwanda 998, idadi kubwa ya viwanda hivyo ilikuwa katika mkoa wa Dar es Salaam, ikiwa na viwanda 376 sawa na asilimia 37.7; ikifuatiwa na mikoa ya Arusha, viwanda 87 (asilimia 8.7); Kagera, viwanda 74 (asilimia 7.4) na mkoa wa Mbeya, viwanda 48 (asilimia 4.8). Mikoa 21 iliyobaki ilikuwa na jumla ya viwanda 413 sawa na asilimia 41.4 ya viwanda vyote katika sekta hii ndogo.

**Mchoro Na. 5: Idadi ya Viwanda Vikubwa Vyenye Wafanyakazi Kumi au Zaidi katika Sekta Ndogo ya Uzalishaji wa Bidhaa Viwandani Ki-Mkoa, Tanzania Bara, CIP 2013**




**Jedwali Na. 2: Idadi ya Viwanda katika Sekta Ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani Ki-Mkoa na Makundi ya Wafanyakazi, Tanzania Bara, CIP 2013**

| Mkoa | Makundi ya Wafanyakazi | | | | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1-4 | 5-9 | 10-19 | 20-49 | 50-99 | 100-499 | 500+ | |
| Dodoma | 1,588 | 199 | 11 | 8 | 2 | 1 | - | 1,809 |
| Arusha | 1,822 | 229 | 30 | 15 | 20 | 17 | 5 | 2,138 |
| Kilimanjaro | 1,483 | 188 | 22 | 11 | 9 | 5 | 1 | 1,719 |
| Tanga | 1,498 | 158 | 13 | 6 | 6 | 11 | 3 | 1,695 |
| Morogoro | 2,599 | 397 | 15 | 15 | 1 | 3 | 7 | 3,037 |
| Pwani | 1,204 | 231 | 8 | 6 | 1 | 4 | 1 | 1,455 |
| Dar es Salaam | 5,763 | 1,233 | 109 | 114 | 65 | 79 | 10 | 7,373 |
| Lindi | 664 | 150 | 6 | - | - | - | - | 820 |
| Mtwara | 866 | 110 | - | 2 | 2 | 2 | - | 982 |
| Ruvuma | 3,257 | 197 | 9 | 4 | - | - | - | 3,467 |
| Iringa | 2,245 | 206 | 9 | 7 | 4 | 5 | 3 | 2,479 |
| Mbeya | 2,527 | 245 | 23 | 18 | 2 | 5 | - | 2,820 |
| Singida | 1,383 | 214 | 21 | 5 | 1 | - | - | 1,624 |
| Tabora | 852 | 83 | 7 | 2 | - | 1 | - | 945 |
| Rukwa | 866 | 61 | 2 | 4 | - | - | - | 933 |
| Kigoma | 836 | 102 | 7 | 1 | - | - | - | 946 |
| Shinyanga | 923 | 225 | 18 | 9 | - | - | - | 1,175 |
| Kagera | 2,042 | 269 | 35 | 30 | 1 | 6 | 2 | 2,385 |
| Mwanza | 1,074 | 279 | 22 | 13 | 8 | 7 | 4 | 1,407 |
| Mara | 2,971 | 517 | 5 | 5 | 2 | 3 | - | 3,503 |
| Manyara | 2,063 | 154 | 12 | 9 | - | - | - | 2,238 |
| Njombe | 1,536 | 116 | - | 4 | 2 | 1 | 1 | 1,660 |
| Katavi | 199 | 20 | - | - | - | - | - | 219 |
| Simiyu | 637 | 109 | 7 | 1 | - | - | - | 754 |
| Geita | 762 | 129 | - | - | - | - | - | 891 |
| **Jumla** | **41,660** | **5,821** | **391** | **289** | **126** | **150** | **37** | **48,474** |

## 2.4 Idadi ya Viwanda katika Makundi ya Wafanyakazi

Kundi lenye wafanyakazi kuanzia mmoja hadi wanne (1-4) lilikuwa na idadi kubwa zaidi ya viwanda (41,919) sawa na asilimia 85.1 ya viwanda vyote (vikubwa na vidogo), likifuatiwa na kundi lenye wafanyakazi kuanzia watano hadi tisa (5-9) lenye viwanda 6,002 sawa na asilimia 12.2 ya viwanda vyote. Hii inaonesha kuwa, viwanda vidogo vyenye mfanyakazi mmoja hadi wafanyakazi tisa (1-9) vilikuwa vingi zaidi kwa kuchangia asilimia 97.3 ya viwanda vyote.

**Mchoro Na. 6: Idadi ya Viwanda kwa Makundi ya Wafanyakazi, Tanzania Bara, CIP 2013**



**Jedwali Na. 3: Idadi ya Viwanda vya Utengenezaji wa Bidhaa kwa shughuli ya Kiwanda na Ukubwa wa Ajira, Tanzania Bara, CIP 2013**

| Shughuli ya Kiwanda | Wafanyakazi Kumi au Zaidi | | Mfanyakazi Mmoja hadi Wafanyakazi Tisa | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia |
| Utengenezaji wa bidhaa za chakula | 382 | 38.3 | 19,315 | 40.7 | 19,697 | 40.6 |
| Utengenezaji wa vinywaji | 47 | 4.8 | 29 | 0.1 | 76 | 0.2 |
| Utengenezaji wa bidhaa za tumbaku | 4 | 0.4 | 10 | 0.0 | 14 | 0.0 |
| Utengenezaji wa nguo | 32 | 3.2 | 676 | 1.4 | 708 | 1.5 |
| Utengenezaji wa mavazi | 13 | 1.3 | 13,280 | 28.0 | 13,293 | 27.4 |
| Utengenezaji wa ngozi na bidhaa zinazohusiana | 18 | 1.7 | 159 | 0.3 | 177 | 0.4 |
| Utengenezaji wa mbao na bidhaa zitokanazo na mbao, fomaika, isipokuwa samani; utengenezaji wa bidhaa zinazotokana na mabua na malighafi za kusukia | 68 | 6.8 | 1,702 | 3.6 | 1,770 | 3.7 |
| Utengenezaji wa karatasi na bidhaa za karatasi | 12 | 1.2 | 6 | 0.0 | 18 | 0.0 |
| Upigaji chapa na uandaaji wa media zilizonakiliwa | 48 | 4.8 | 120 | 0.3 | 168 | 0.3 |
| Utengenezaji wa makaa ya mawe na bidhaa za mafuta ya petroli iliyosafishwa | 3 | 0.3 | 0 | 0.0 | 3 | 0.0 |
| Utengenezaji kemikali na bidhaa za kemikali | 40 | 3.9 | 48 | 0.1 | 88 | 0.2 |
| Utengenezaji wa madawa ya binadamu, kemikali za kutibia na bidhaa za mimea | 5 | 0.5 | 2 | 0.0 | 7 | 0.0 |
| Utengenezaji wa bidhaa za mpira na plastiki | 42 | 4.3 | 22 | 0.0 | 64 | 0.1 |
| Utengenezaji wa bidhaa nyingine za madini zisizo za metali | 89 | 8.8 | 1,014 | 2.1 | 1,103 | 2.3 |
| Utengenezaji wa metali za msingi | 14 | 1.4 | 5 | 0.0 | 19 | 0.0 |
| Utengenezaji wa bidhaa za metali, isipokuwa mitambo na vifaa | 54 | 5.4 | 3,751 | 7.9 | 3,805 | 7.8 |
| Utengenezaji wa kompyuta, vifaa vya kielektroniki na uoni | 1 | 0.1 | 1 | 0.0 | 2 | 0.0 |
| Utengenezaji wa vifaa vya umeme | 20 | 2.0 | 233 | 0.5 | 253 | 0.5 |
| Utengenezaji wa mashine/mitambo na vifaa ambavyo havijatajwa | 14 | 1.5 | 85 | 0.2 | 99 | 0.2 |
| Utengenezaji wa magari na matela ya malori | 13 | 1.4 | 24 | 0.0 | 37 | 0.1 |
| Utengenezaji wa vyombo vingine vya usafiri | 2 | 0.2 | 45 | 0.1 | 47 | 0.1 |
| Utengenezaji wa samani | 60 | 6.0 | 6,763 | 14.2 | 6,823 | 14.1 |
| Utengenezaji mwingine wa bidhaa za viwandani | 13 | 1.3 | 162 | 0.3 | 175 | 0.4 |
| Ukarabati na ufungaji wa mitambo na vifaa | 4 | 0.4 | 24 | 0.1 | 28 | 0.1 |
| **Jumla** | **998** | **100.0** | **47,476** | **100.0** | **48,474** | **100.0** |

## 2.5 Idadi ya Viwanda Kulingana na Aina ya Umiliki

Kutoka jumla ya viwanda 49,243, viwanda 48,975 sawa na asilimia 99.4 vilimilikiwa na mashirika binafsi, viwanda 238 sawa na asilimia 0.5 vilimilikiwa na Serikali, wakati viwanda 30 sawa na asilimia 0.1 vilimilikiwa kwa ubia kati ya Serikali na mashirika binafsi. Matokeo pia yanaonesha kuwa, kati ya viwanda vikubwa, asilimia 86.5 ni vya mashirika binafsi, asilimia 11.4 ni vya Serikali na asilimia mbili (2) ni viwanda vyenye ubia kati ya Serikali na mashirika binafsi. Kwa ujumla, karibu viwanda vyote vidogo vilikuwa vya umiliki wa mashirika binafsi kwa asilimia 99.8.

**Jedwali Na. 4: Idadi ya Viwanda Kulingana na Aina ya Umiliki**

| Aina ya Umiliki | Wafanyakazi kumi au Zidi | | Mfanyakazi Mmoja Hadi Wafanyakazi Tisa | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia |
| Serikali | 151 | 11.4 | 87 | 0.2 | 238 | 0.5 |
| Mashirika Binafsi | 1,144 | 86.5 | 47,831 | 99.8 | 48,975 | 99.4 |
| Ubia | 27 | 2.0 | 3 | 0.0 | 30 | 0.1 |
| **Jumla** | **1,322** | **100.0** | **47,921** | **100.0** | **49,243** | **100.0** |

## 2.6 Idadi ya Viwanda kwa Msingi wa Umiliki Kisheria

Kuendana na msingi wa umiliki wa kisheria, matokeo yanaonesha kuwa, katika jumla ya viwanda 49,243, umiliki wa mtu mmoja ulikuwa na viwanda 44,748 sawa na asilimia 90.9, ikifuatiwa na ubia, viwanda 3,388 (asilimia 6.9) na mashirika binafsi yenye hisa za dhima isiyo na ukomo, viwanda 416 (asilimia 0.8). Umiliki wa misingi mingine ya kisheria ilihusisha viwanda 693 sawa na asilimia 1.4 ya viwanda vyote.

Kuhusu idadi ya viwanda vikubwa vyenye wafanyakazi kumi au zaidi, ambavyo vilikuwa 1,322, umiliki wa msingi kisheria ni kama ifuatavyo: mashirika binafsi yenye hisa za dhima isiyo na ukomo yalikuwa na viwanda 374 (asilimia 28.3) ikifuatiwa na umiliki wa mtu mmoja 372 (asilimia 28.1) na ubia viwanda 353 (asilimia 26.7). Misingi mingine ya kisheria ilihusisha viwanda 223 sawa na asilimia 16.9 ya viwanda vyote vikubwa.

Kuhusu viwanda vidogo vyenye mfanyakazi mmoja hadi wafanyakazi tisa vipatavyo 47,921, umiliki kwa msingi kisheria ilikuwa kama ifuatavyo: umiliki wa mtu mmoja ulikuwa na viwanda 44,374 sawa na asilimia 92.6, ikifuatiwa na ubia, viwanda 3,035 (asilimia 6.3); na ushirika, viwanda 315 (asilimia 0.7). Umiliki wa misingi mingine kisheria ilihusisha viwanda 198 sawa na asilimia 0.4 ya viwanda vyote vidogo.

**Jedwali Na. 5: Idadi ya Viwanda kwa Msingi wa Umiliki Kisheria na Ukubwa wa Ajira, Tanzania Bara, CIP 2013**

| Msingi wa Umiliki Kisheria | Viwanda Vyenye Wafanyakazi Kumi au Zaidi | | Viwanda Vyenye Mfanyakazi Mmoja Hadi Wafanyakazi Tisa | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Idadi** | **Asilimia** | **Idadi** | **Asilimia** | **Idadi** | **Asilimia** |
| Umiliki wa Mtu mmoja | 372 | 28.1 | 44,376 | 92.6 | 44,748 | 90.9 |
| Ubia | 353 | 26.7 | 3,035 | 6.3 | 3,388 | 6.9 |
| Umma | 87 | 6.6 | 60 | 0.1 | 147 | 0.3 |
| Shirika la Umma | 36 | 2.7 | 3 | 0.0 | 39 | 0.1 |
| Ushirika | 48 | 3.6 | 315 | 0.7 | 363 | 0.7 |
| Shirika Binafsi ya hisa za dhima isiyo na ukomo | 42 | 3.2 | 5 | 0.0 | 47 | 0.1 |
| Shirika Binafsi ya hisa za dhima yenye ukomo | 374 | 28.3 | 42 | 0.1 | 416 | 0.8 |
| Misingi mingine ya umiliki kisheria | 10 | 0.8 | 85 | 0.2 | 95 | 0.2 |
| **Jumla** | **1,322** | **100.0** | **47,921** | **100.0** | **49,243** | **100.0** |

# 3.0 IDADI YA WAFANYAKAZI VIWANDANI

## 3.1 Idadi ya Wafanyakazi Katika Sekta Ndogo za Viwanda

Matokeo yanaonesha kuwa, idadi ya wafanyakazi katika sekta ndogo nne ilikuwa 264,223; kati ya hao, wafanyakazi wa viwanda vilivyojihusisha na utengenezaji wa bidhaa viwandani walikuwa 231,099 (asilimia 87.5), ikifuatiwa na sekta ndogo ya uchimbaji madini na mawe yenye wafanyakazi 19,906 (asilimia 7.5). Sekta ndogo mbili zilizobaki (umeme na maji) zilikuwa ni asilimia 5.0 ya wafanyakazi wote viwandani.

Aidha, viwanda vikubwa vyenye wafanyakazi kumi au zaidi vilikuwa na wafanyakazi 138,887 (asilimia 52.5) na vidogo vyenye mfanyakazi mmoja hadi wafanyakazi tisa vilikuwa na wafanyakazi 125,336 (asilimia 47.5). Matokeo yanaonesha kwamba, sekta ndogo ya viwanda ndiyo iliyoongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya wafanyakazi kwa viwanda vidogo na vikubwa kwa asilimia 76.6 na 98.4 kwa mtiririko huo.

**Jedwali Na. 6: Idadi ya Wafanyakazi kwa Sekta Ndogo za Viwanda na Ukubwa wa Ajira, Tanzania Bara, CIP 2013**

| Sekta Ndogo | Viwanda Vyenye Wafanyakazi Kumi au Zaidi | | Viwanda Vyenye Mfanyakazi Mmoja Hadi Wafanyakazi Tisa | | Jumla | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia | Idadi | Asilimia |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 18,917 | 13.6 | 989 | 0.8 | 19,907 | 7.5 |
| Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani | 107,733 | 77.6 | 123,366 | 98.4 | 231,099 | 87.5 |
| Uzalishaji na Usambazaji wa Umeme, Gesi, Mvuke na kubadilisha hali(joto/baridi) | 7,915 | 5.7 | 335 | 0.3 | 8,250 | 3.1 |
| Kukusanya, kutibu na kusambaza maji | 4,322 | 3.1 | 646 | 0.5 | 4,968 | 1.9 |
| **Jumla** | **138,887** | **100.0** | **125,336** | **100.0** | **264,223** | **100.0** |

## 3.2 Idadi ya Wafanyakazi Kijinsia Katika Sekta Ndogo za Viwanda

Matokeo yanaonesha kuwa, viwanda vikubwa vyenye wafanyakazi kumi au zaidi; sekta ndogo ya uchimbaji madini na mawe ilikuwa na wafanyakazi wanaume 17,702 ambao ni asilimia 93.6 na wanawake 1,215 ikiwa ni asilimia 6.4 ya wafanyakazi wote katika sekta hiyo; sekta ndogo ya viwanda ilikuwa na wafanyakazi wanaume 75,791 ambao ni asilimia 70.4 na wanawake 31,942 ikiwa ni asilimia 29.6; umeme, gesi, mvuke na hali ya hewa wafanyakazi wanaume 6,690 ambao ni asilimia 84.5 na wanawake 1,225 asilimia 15.5; na sekta ndogo ya kukusanya, kutibu na kusambaza maji, wafanyakazi wanaume 3,348 ambao ni asilimia 77.5 na wanawake 974 ikiwa ni asilimia 22.5. Kwa ujumla, viwanda vikubwa vilikuwa na wafanyakazi wengi wanaume 103,531 (asilimia 74.5) kuliko wanawake 35,356 (asilimia 25.5%).

Kwa upande wa viwanda vidogo vyenye mfanyakazi mmoja hadi wafanyakazi tisa, matokeo yanaonesha kuwa, sekta ndogo ya uchimbaji madini na mawe ilikuwa na wafanyakazi wanaume 759 ambao ni asilimia 76.7 na wanawake 230 sawa na asilimia 23.2 ya wafanyakazi wote; utengenezaji wa bidhaa viwandani, wafanyakazi wanaume walikuwa 98,001 ikiwa ni asilimia 79.4 na wanawake 25,365 sawa na asilimia 20.6; umeme, gesi, mvuke na kubadilisha hali ya hewa (joto na baridi), wafanyakazi wanaume 310 ambao ni asilimia 92.5 na wanawake 25 sawa na asilimia 7.5; kukusanya, kutibu na kusambaza maji, wanaume 435 (asilimia 67.5) na wanawake 209 (asilimia 32.5). Hali hii inafanana na ile ya viwanda vikubwa kwa kuwa na wafanyakazi wengi wanaume 99,507 (asilimia 79.4) kuliko wanawake 25,829 (asilimia 20.6).

Kwa ujumla, Sekta ya Viwanda ilikuwa na wafanyakazi 264,223 ambao kati yao; wafanyakazi 203,038 sawa na asilimia 76.8 ni wanaume na wafanyakazi 61,185 sawa na asilimia 23.2 ni wanawake.

**Jedwali Na. 7: Idadi ya Wafanyakazi Kijinsi kwa Sekta Ndogo za Viwanda na Ukubwa wa Ajira, Tanzania Bara, CIP 2013**

| Sekta Ndogo | Viwanda Vyenye Wafanyakazi Kumi au Zaidi | | | Viwanda Vyenye Mfanyakazi Mmoja Hadi Wafanyakazi Tisa | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Me | Ke | Jumla | Me | Ke | Jumla |
| Uchimbaji Madini na Mawe | 17,702 | 1,215 | 18,917 | 759 | 230 | 989 |
| Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani | 75,791 | 31,942 | 107,733 | 98,001 | 25,365 | 123,366 |
| Uzalishaji na usambazaji wa Umeme, Gesi, Mvuke na kubadilisha hali(joto/baridi) | 6,690 | 1,225 | 7,915 | 310 | 25 | 335 |
| Kukusanya, kutibu na kusambaza maji | 3,348 | 974 | 4,322 | 436 | 209 | 646 |
| **Jumla** | **103,531** | **35,356** | **138,887** | **99,507** | **25,829** | **125,336** |

## 3.3 Idadi ya Wafanyakazi kwa Shughuli za Viwanda

Idadi ya wafanyakazi katika shughuli za viwanda hutofautiana kutoka shughuli moja hadi nyingine kwa mwaka 2013 ambapo idadi ya wafanyakazi katika viwanda ilikuwa 264,223. Shughuli kuu tatu za viwanda zilikuwa na asilimia 52.8 ya wafanyakazi hao, kama ifuatavyo: utengenezaji wa bidhaa za chakula, wafanyakazi 85,330 sawa na asilimia 32.3, utengenezaji wa bidhaa za mavazi, wafanyakazi 30,539 sawa na asilimia 11.6, na utengenezaji wa samani wafanyakazi 23,740 sawa na asilimia 9.0. Shughuli nyingine za viwanda zimechangia jumla ya wafanyakazi 124,616 sawa na asilimia 47.2 ya wafanyakazi wote viwandani.


**Jedwali Na. 8: Idadi ya Wafanyakazi kwa Shughuli za Viwanda, Tanzania Bara, CIP 2013**

| Shughuli ya Kiwanda | Idadi ya Wafanyakazi | Asilimia |
|---|---|---|
| Utengenezaji wa bidhaa za chakula | 85,330 | 32.3 |
| Utengenezaji wa mavazi | 30,539 | 11.6 |
| Utengenezaji wa samani | 23,740 | 9.0 |
| Utengenezaji wa nguo | 17,714 | 6.7 |
| Utengenezaji wa bidhaa za metali, ispokuwa mitambo na vifaa | 14,889 | 5.6 |
| Uchimbaji wa madini mengine na mawe | 9,988 | 3.8 |
| Uchimbaji wa metali ghafi | 9,843 | 3.7 |
| Utengenezaji wa mbao na bidhaa zitokanazo na mbao, fomaika, isipokuwa samani; utengenezaji wa bidhaa zinazotokana na mabua na malighafi za kusukia | 9,418 | 3.6 |
| Utengenezaji wa bidhaa zingine za madini zisizo za metali | 9,384 | 3.6 |
| Uzalishaji na usambazaji wa umeme, gesi, mvuke na kubadilisha hali(joto/baridi) | 8,250 | 3.1 |
| Utengenezaji wa vinywaji | 7,004 | 2.7 |
| Utengenezaji kemikali na bidhaa za kemikali | 6,645 | 2.5 |
| Utengenezaji wa bidhaa za tumbaku | 5,110 | 1.9 |
| Kukusanya, kutibu na kusambaza maji | 4,725 | 1.8 |
| Utengenezaji wa bidhaa za mpira na plastiki | 4,342 | 1.6 |
| Upigaji chapa na Uandaaji wa media zilizonakiliwa | 3,339 | 1.3 |
| Utengenezaji wa karatasi na bidhaa za karatasi | 2,253 | 0.9 |
| Utengenezaji wa metali za msingi | 2,194 | 0.8 |
| Utengenezaji wa vifaa vya umeme | 1,742 | 0.7 |
| Utengenezaji wa ngozi na bidhaa zinazohusiana | 1,725 | 0.7 |
| Utengenezaji mwingine wa bidhaa vya viwandani | 1,709 | 0.6 |
| Utengenezaji wa magari na matela ya malori | 1,391 | 0.5 |
| Utengenezaji wa madawa ya binadamu, kemikali za kutibia na bidhaa za mimea | 790 | 0.3 |
| Utengenezaji wa mashine/mitambo na vifaa ambavyo havijatajwa | 726 | 0.3 |
| Ukarabati na ufungaji wa mitambo na vifaa | 417 | 0.2 |
| Utengenezaji wa vyombo vingine vya usafiri | 330 | 0.1 |
| Utengenezaji wa makaa ya mawe na bidhaa za mafuta ya petroli iliyosafishwa | 243 | 0.1 |
| Ukusanyaji taka, shughuli za kutibu na kutupa taka; urejeshaji nyenzo | 242 | 0.1 |
| Utengenezaji wa kompyuta, vifaa vya kielektroniki na uoni | 124 | 0.0 |
| Uchimbaji wa Makaa ya mawe magumu na mepesi | 77 | 0.0 |
| **Jumla** | **264,223** | **100.0** |

## 3.4 Idadi ya Wafanyakazi Ki-Mkoa

Mkoa wa Dar es Salaam ulikuwa na wafanyakazi wengi kuliko mikoa mingine ambao ni 60,754 (asilimia 23.0) ikifuatiwa na Morogoro, 24,001 (asilimia 9.1); Arusha 17,701 (asilimia 6.7); Tanga 14,618 (asilimia 5.5); Kagera 14,614 (asilimia 5.5); Mara 14,418 (asilimia 5.5) na Manyara wafanyakazi 12,023 (asilimia 4.5). Mkoa wa Katavi ulikuwa na wafanyakazi wachache kuliko mikoa mingine kwa kuwa na wafanyakazi ambao ni 526 (asilimia 0.2). Mikoa iliyobaki idadi ya wafanyakazi ni kama inavyoonekana katika mchoro namba saba (7).


**Mchoro Na. 7: Idadi ya Wafanyakazi Ki-Mkoa, Tanzania Bara, CIP 2013**



## 3.5 Idadi ya Wafanyakazi Katika Sekta Ndogo za Viwanda

Viwanda vidogo vyenye mfanyakazi mmoja hadi wafanyakazi wanne vilikuwa na idadi kubwa ya wafanyakazi 86,960 (asilimia 32.9) vikifuatiwa na viwanda vyenye wafanyakazi 500 au zaidi 64,384 (asilimia 24.4); na viwanda vyenye wafanyakazi 100 hadi 499 vilikuwa na wafanyakazi 43,363 (asilimia 16.4). Viwanda vyenye wafanyakazi 10 hadi 19 vilikuwa na wafanyakazi wachache, 6,767 (asilimia 2.6) kuliko makundi mengine.

**Mchoro Na. 8: Asilimia ya Wafanyakazi kwa Makundi ya Wafanyakazi, Tanzania Bara, CIP 2013**



# 4.0 MALIPO KWA WAFANYAKAZI

## 4.1 Malipo kwa Wafanyakazi Katika Sekta Ndogo za Viwanda

Malipo kwa wafanyakazi yanahusu jumla ya malipo kwa wafanyakazi wote kwa fedha taslimu au fadhila, yanajumuisha mishahara, malipo ya muda wa ziada, gharama za usafiri, michango kwa mfanyakazi kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na malipo ya ziada kwa kuchangia uzalishaji katika kipindi husika.

Matokeo yameonesha kuwa, jumla ya malipo kwa wafanyakazi viwandani mwaka 2013 yalifikia Shilingi milioni 1,366,744. Malipo makubwa zaidi yalitolewa katika sekta ndogo ya utengenezaji wa bidhaa viwandani yaliyogharimu Shilingi milioni 791,311 sawa na asilimia 57.9 ya gharama zote kwa wafanyakazi; yakifuatiwa na sekta ndogo ya madini na uchimbaji mawe Shillingi millioni 364,299 sawa na asilimia 26.7; na sekta ndogo ya umeme, gesi, mvuke na kubadilisha hali ya hewa Shilingi milioni 181,050 sawa na asilimia 13.2. Sekta ndogo ya kukusanya, kutibu na kusambaza maji yaligharimu Shilingi milioni 30,084 sawa na asilimia 2.2 ya malipo yote ya kazi viwandani.

Matokeo pia yanaonesha kuwa, viwanda vikubwa vililipa jumla ya malipo ya Shilingi milioni 1,253,835 sawa na asilimia 91.7 wakati viwanda vidogo vililipa jumla ya Shilingi milioni 112,909 sawa na asilimia 8.3 ya malipo yote ya kazi. Viwanda vya sekta ndogo ya utengenezaji wa bidhaa viwandani yaliongoza katika viwanda vikubwa na vidogo. Katika viwanda vikubwa, jumla ya malipo yalikuwa Shilingi milioni 680,428 sawa na asilimia 54.3 ya malipo wakati viwanda vidogo vililipa jumla ya Shilingi milioni 110,883 sawa na asilimia 98.2 ya malipo ya kazi katika sekta ndogo husika.

**Jedwali Na. 9: Malipo kwa Wafanyakazi Katika Sekta Ndogo za Viwanda na Ukubwa wa Ajira, Tanzania Bara, CIP 2013**

**(Shilingi Milioni)**

| Sekta Ndogo | Viwanda Vyenye Wafanyakazi Kumi au Zaidi | Viwanda Vyenye Mfanyakazi Mmoja Hadi Wafanyakazi Tisa | Jumla |
|---|---|---|---|
| Uchimbaji Madini na Mawe | 363,111 | 1,188 | 364,299 |
| Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani | 680,428 | 110,883 | 791,311 |
| Uzalishaji na usambazaji wa Umeme, Gesi, Mvuke na kubadilisha hali(joto/baridi) | 180,794 | 256 | 181,050 |
| Kukusanya, kutibu na kusambaza maji | 29,502 | 582 | 30,084 |
| **Jumla** | **1,253,835** | **112,909** | **1,366,744** |

## 5.0 ONGEZEKO LA THAMANI

Ongezeko la Thamani ni mrejesho unaotokana na shughuli za uzalishaji mali, ambao ni tofauti kati ya Pato Ghafi (Gross Output) na Gharama za Uzalishaji (Intermediate Consumption). Ni kipimo cha mchango wa kiwanda husika katika Pato la Taifa (Gross Domestic Product - GDP).

### 5.1 Ongezeko la Thamani katika Sekta Ndogo za Viwanda

Matokeo yanaonesha kuwa, jumla ya ongezeko la thamani kwa sekta yote ya viwanda ni Shilingi milioni 8,220,560. Viwanda vikubwa vyenye wafanyakazi kumi au zaidi vilikuwa na ongezeko la thamani la Shilingi milioni 7,857,680, sawa na asilimia 95.6 ya jumla ya ongezeko la thamani. Ambapo mchango wa viwanda vidogo vyenye wafanyakazi mmoja hadi wafanyakazi tisa ulikuwa ni Shilingi milioni 362,880, sawa na asilimia 4.4 ya ongezeko la thamani kwa viwanda vyote.

Kama kawaida, sekta ndogo ya utengenezaji bidhaa viwandani iliongoza kwa kuwa na mchango mkubwa zaidi wa Shilingi milioni 4,907,991, sawa na asilimia 59.7 ya jumla ya ongezeko la thamani viwandani. Viwanda vikubwa vilichangia Shilingi milioni 4,552,716 sawa na asilimia 92.8 ya sekta hii ndogo.

Sekta ndogo iliyofuatia kwa mchango mkubwa ilikuwa ya uchimbaji madini na mawe iliyochangia Shilingi milioni 2,920,392, sawa na asilimia 35.5 ya ongezeko la thamani viwandani; ikifuatiwa na uzalishaji na usambazaji wa umeme, gesi, mvuke na kubadilishaji hali ya hewa iliyochangia Shilingi milioni 311,730, sawa na asilimia 3.8 ya ongezeko la thamani viwandani. Sekta ndogo ya kukusanya, kutibu na kusambaza maji ilikuwa na mchango mdogo kuliko mingine, kwa kuchangia Shilingi milioni 80,447 sawa na asilimia 1.0 ya ongezeko la thamani yote viwandani.

**Jedwali Na. 10: Ongezeko la Thamani kwa Sekta Ndogo za Viwanda na ukubwa wa Ajira, Tanzania Bara, CIP 2013**

**(Shilingi Milioni)**

| Sekta Ndogo | Viwanda Vyenye Wafanyakazi Kumi au Zaidi | Viwanda Vyenye Mfanyakazi Mmoja Hadi Wafanyakazi Tisa | Jumla |
|---|---|---|---|
| Uchimbaji Madini na Mawe | 2,915,516 | 4,876 | 2,920,392 |
| Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani | 4,552,716 | 355,275 | 4,907,991 |
| Uzalishaji na usambazaji wa Umeme, Gesi, Mvuke na kubadilisha hali(joto/baridi) | 310,910 | 820 | 311,730 |
| Kukusanya, kutibu na kusambaza maji | 78,538 | 1,909 | 80,447 |
| **Jumla** | **7,857,680** | **362,880** | **8,220,560** |

## 5.2 Ongezeko la Thamani Katika Shughuli za Viwanda

Ongezeko la thamani lilitofautiana kati ya shughuli moja hadi nyingine. Kwa viwanda vikubwa vilivyokuwa na wafanyakazi kumi au zaidi, shughuli za uchimbaji wa metali ghafi ziliongoza kwa kuwa na ongezeko la thamani la Shilingi milioni 2,796,275 (asilimia 35.6); ikifuatiwa na utengenezaji wa bidhaa za chakula kwa ongezeko la thamani la Shilingi milioni 1,760,221 (asilimia 22.4). Utengenezaji wa vinywaji ongezeko lilikuwa Shilingi milioni 1,019,260 (asilimia 13.0); na utengenezaji wa bidhaa za tumbaku ongezeko lilikuwa Shilingi milioni 409,867 (asilimia 5.2). Viwanda vingine vilichangia jumla ya Shilingi milioni 1,872,057 sawa na asilimia 23.8 ya ongezeko la thamani yote viwandani.

**Jedwali Na. 11: Ongezeko la Thamani kwa Shughuli za Viwanda na Ukubwa wa Ajira, Tanzania Bara, CIP 2013**

**(Shilingi Milioni)**

| Shughuli ya Kiwanda | Viwanda Vyenye Wafanyakazi Kumi au Zaidi | Viwanda Vyenye Mfanyakazi Mmoja Hadi Wafanyakazi Tisa | Jumla |
|---|---|---|---|
| Uchimbaji wa Makaa ya mawe magumu na mepesi | 393 | 0 | 393 |
| Uchimbaji wa metali ghafi | 2,796,275 | 1,006 | 2,797,281 |
| Uchimbaji wa madini mengine na mawe | 118,848 | 3,870 | 122,718 |
| Utengenezaji wa bidhaa za chakula | 1,760,221 | 148,297 | 1,908,518 |
| Utengenezaji wa vinywaji | 1,019,260 | 1,051 | 1,020,311 |
| Utengenezaji wa bidhaa za tumbaku | 409,867 | 71 | 409,938 |
| Utengenezaji wa nguo | 163,733 | 3,749 | 167,482 |
| Utengenezaji wa mavazi | 10,050 | 54,189 | 64,239 |
| Utengenezaji wa ngozi na bidhaa zinazohusiana | 13,965 | 1,439 | 15,404 |
| Utengenezaji wa mbao na bidhaa zitokanazo na mbao, fomaika, isipokuwa samani; utengenezaji wa bidhaa zinazotokana na mabua na malighafi za kusukia | 67,907 | 18,865 | 86,772 |
| Utengenezaji wa karatasi na bidhaa za karatasi | 16,319 | 101 | 16,420 |
| Upigaji chapa na uandaaji wa media zilizonakiliwa | 69,475 | 3,490 | 72,965 |
| Utengenezaji wa makaa ya mawe na bidhaa za mafuta ya petroli iliyosafishwa | 15,060 | 0 | 15,060 |
| Utengenezaji kemikali na bidhaa za kemikali | 171,859 | 959 | 172,818 |
| Utengenezaji wa madawa ya binadamu, kemikali za kutibia na bidhaa za mimea | 19,580 | 13 | 19,593 |
| Utengenezaji wa bidhaa za mpira na plastiki | 186,043 | 591 | 186,634 |
| Utengenezaji wa bidhaa zingine za madini zisizo za metali | 306,985 | 25,133 | 332,118 |
| Utengenezaji wa metali za msingi | 32,589 | 61 | 32,650 |
| Utengenezaji wa bidhaa za metali, isipokuwa mitambo na vifaa | 36,204 | 36,360 | 72,564 |
| Utengenezaji wa kompyuta, vifaa vya kielektroniki na uoni | 30,967 | 29 | 30,996 |
| Utengenezaji wa vifaa vya umeme | 22,315 | 2,571 | 24,886 |
| Utengenezaji wa mashine/mitambo na vifaa ambavyo havijatajwa | 4,248 | 2,173 | 6,421 |
| Utengenezaji wa magari na matela ya malori | 16,222 | 690 | 16,912 |
| Utengenezaji wa vyombo vingine vya usafiri | 13,883 | 265 | 14,148 |
| Utengenezaji wa samani | 107,416 | 52,568 | 159,984 |
| Utengenezaji mwingine wa bidhaa za viwandani | 26,683 | 2,191 | 28,874 |
| Ukarabati na ufungaji wa mitambo na vifaa | 31,864 | 421 | 32,285 |
| Uzalishaji na usambazaji wa umeme, gesi, mvuke na kubadilisha hali (joto/baridi) | 310,910 | 820 | 311,730 |
| Kukusanya, kutibu na kusambaza maji | 75,844 | 1,803 | 77,647 |
| Ukusanyaji taka, shughuli za kutibu na kutupa taka; urejeshaji nyenzo | 2,694 | 106 | 2,800 |
| **Jumla** | **7,857,679** | **362,882** | **8,220,561** |

**Jedwali Na. 12: Ongezeko la Thamani kwa Sekta Ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani, Tanzania Bara, CIP 2013**

**(Shilingi Milioni)**

| **Shughuli ya Kiwanda** | **Viwanda vyenye wafanyakazi kumi au zaidi** | | |
|---|---|---|---|
| | **Pato Ghafi** | **Gharama za Uzalishaji** | **Ongezeko la Thamani** |
| Utengenezaji wa bidhaa za chakula | 3,953,075 | 2,192,855 | 1,760,220 |
| Utengenezaji wa vinywaji | 1,743,089 | 723,829 | 1,019,260 |
| Utengenezaji wa bidhaa za tumbaku | 655,603 | 245,736 | 409,867 |
| Utengenezaji wa nguo | 404,590 | 240,857 | 163,733 |
| Utengenezaji wa mavazi | 24,619 | 14,570 | 10,049 |
| Utengenezaji wa ngozi na bidhaa zinazohusiana | 55,042 | 41,077 | 13,965 |
| Utengenezaji wa mbao na bidhaa zitokanazo na mbao, fomaika, isipokuwa samani; utengenezaji wa bidhaa zinazotokana na mabua na malighafi za kusukia | 124,421 | 56,514 | 67,907 |
| Utengenezaji wa karatasi na bidhaa za karatasi | 96,703 | 80,384 | 16,319 |
| Upigaji chapa na uandaaji wa media zilizonakiliwa | 177,532 | 108,057 | 69,475 |
| Utengenezaji wa makaa ya mawe na bidhaa za mafuta ya petroli iliyosafishwa | 70,052 | 54,992 | 15,060 |
| Utengenezaji kemikali na bidhaa za kemikali | 554,111 | 382,252 | 171,859 |
| Utengenezaji wa madawa ya binadamu, kemikali za kutibia na bidhaa za mimea | 60,170 | 40,590 | 19,580 |
| Utengenezaji wa bidhaa za mpira na plastiki | 631,542 | 445,498 | 186,044 |
| Utengenezaji wa bidhaa zingine za madini zisizo za metali | 759,228 | 452,242 | 306,986 |
| Utengenezaji wa metali za msingi | 170,807 | 138,218 | 32,589 |
| Utengenezaji wa bidhaa za metali, isipokuwa mitambo na vifaa | 115,917 | 79,713 | 36,204 |
| Utengenezaji wa kompyuta, vifaa vya kielektroniki na uoni | 36,456 | 5,488 | 30,968 |
| Utengenezaji wa vifaa vya umeme | 102,967 | 80,652 | 22,315 |
| Utengenezaji wa mashine/mitambo na vifaa ambavyo havijatajwa | 10,393 | 6,145 | 4,248 |
| Utengenezaji wa magari na matela ya malori | 38,856 | 22,634 | 16,222 |
| Utengenezaji wa vyombo vingine vya usafiri | 60,480 | 46,597 | 13,883 |
| Utengenezaji wa samani | 369,046 | 261,629 | 107,417 |
| Utengenezaji mwingine wa bidhaa za viwandani | 70,301 | 43,618 | 26,683 |
| Ukarabati na ufungaji wa mitambo na vifaa | 34,946 | 3,081 | 31,865 |
| **Jumla** | **10,319,946** | **5,767,228** | **4,552,718** |

**Jedwali Na. 13: Mgawanyo wa Ongezeko la Thamani Katika Viwanda vya Utengenezaji Bidhaa Viwandani kwa Makundi ya Wafanyakazi, Tanzania Bara, CIP 2013**

| **Kundi la Wafanyakazi** | **Shilingi Milioni** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| 1-9 | 355,275 | 7.2 |
| 10 -19 | 152,800 | 3.1 |
| 20 - 49 | 182,357 | 3.7 |
| 50 – 99 | 336,860 | 6.9 |
| 100 - 499 | 1,758,339 | 35.8 |
| 500+ | 2,122,361 | 43.2 |
| **Jumla** | **4,907,992** | **100.0** |

**Jedwali Na. 14: Ongezeko la Thamani katika Secta Ndogo ya Utengenezaji wa Bidhaa Viwandani, Tanzania Bara, CIP 2013**

**(Shilingi Milioni)**

| **Shughuli ya Kiwanda** | **Viwanda vyenye Mfanyakazi Mmoja Hadi Wafanyakazi Tisa** | | |
|---|---|---|---|
| | **Pato Ghafi** | **Gharama za Uzalishaji** | **Ongezeko la Thamani** |
| Utengenezaji wa bidhaa za chakula | 278,054 | 129,757 | 148,297 |
| Utengenezaji wa vinywaji | 1,822 | 771 | 1,051 |
| Utengenezaji wa bidhaa za tumbaku | 104 | 33 | 71 |
| Utengenezaji wa nguo | 6,084 | 2,335 | 3,749 |
| Utengenezaji wa mavazi | 76,725 | 22,536 | 54,189 |
| Utengenezaji wa ngozi na bidhaa zinazohusiana | 2,425 | 986 | 1,439 |
| Utengenezaji wa mbao na bidhaa zitokanazo na mbao, fomaika, isipokuwa samani; utengenezaji wa bidhaa zinazotokana na mabua na malighafi za kusukia | 31,142 | 12,277 | 18,865 |
| Utengenezaji wa karatasi na bidhaa za karatasi | 185 | 84 | 101 |
| Upigaji chapa na Uandaaji wa media zilizonakiliwa | 6,808 | 3,318 | 3,490 |
| Utengenezaji kemikali na bidhaa za kemikali | 1,670 | 711 | 959 |
| Utengenezaji wa madawa ya binadamu, kemikali za kutibia na bidhaa za mimea | 23 | 10 | 13 |
| Utengenezaji wa bidhaa za mpira na plastiki | 1,180 | 590 | 590 |
| Utengenezaji wa bidhaa zingine za madini zisizo za metali | 48,697 | 23,563 | 25,134 |
| Utengenezaji wa metali za msingi | 109 | 48 | 61 |
| Utengenezaji wa bidhaa za metali, isipokuwa mitambo na vifaa | 63,530 | 27,171 | 36,359 |
| Utengenezaji wa kompyuta, vifaa vya kielektroniki na uoni | 97 | 68 | 29 |
| Utengenezaji wa vifaa vya umeme | 4,008 | 1,438 | 2,570 |
| Utengenezaji wa mashine/mitambo na vifaa ambavyo havijatajwa | 3,653 | 1,480 | 2,173 |
| Utengenezaji wa magari na matela ya malori | 1,246 | 557 | 689 |
| Utengenezaji wa vyombo vingine vya usafiri | 586 | 321 | 265 |
| Utengenezaji wa samani | 83,571 | 31,004 | 52,567 |
| Utengenezaji mwingine wa bidhaa za viwandani | 4,493 | 2,301 | 2,192 |
| Ukarabati na ufungaji wa mitambo na vifaa | 639 | 217 | 422 |
| **Jumla** | **616,851** | **261,576** | **355,275** |

## 5.3 Ongezeko la Thamani Ki-Mkoa

Mkoa wa Dar es Salaam ulichangia kiasi kikubwa zaidi ya mikoa mingine Shilingi milioni 2,268,952 (asilimia 27.6) ikifuatiwa na Morogoro Shilingi milioni 1,038,188 (asilimia 12.6); Mara Shilingi milioni 1,029,078 (asilimia 12.5); Shinyanga Shilingi milioni 896,788 (asilimia 10.9); na Geita

Shilingi milioni 837,068 (asilimia 10.2). Mikoa hii mitano ilichangia jumla ya Shilingi milioni 6,070,074 (asilimia 73.8) ya ongezeko la thamani viwandani. Mikoa 20 iliyobaki ilichangia jumla ya Shilingi milioni 2,150,488 sawa na asilimia 26.2 ya ongezeko la thamani yote viwandani.

**Jedwali Na. 15: Ongezeko la Thamani kwa Mkoa na Ukubwa wa Ajira, Tanzania Bara, CIP 2013**

**(Shilingi Milioni)**

| Mkoa | Viwanda Vyenye Wafanyakazi Kumi au Zaidi | Viwanda Vyenye Mfanyakazi Mmoja Hadi Wafanyakazi Tisa | Jumla |
|---|---:|---:|---:|
| Dodoma | 21,399 | 16,289 | 37,688 |
| Arusha | 354,046 | 19,042 | 373,088 |
| Kilimanjaro | 238,685 | 10,198 | 248,883 |
| Tanga | 264,782 | 12,056 | 276,838 |
| Morogoro | 1,008,892 | 29,296 | 1,038,188 |
| Pwani | 22,775 | 10,135 | 32,910 |
| Dar es Salaam | 2,170,810 | 98,142 | 2,268,952 |
| Lindi | 3,017 | 4,856 | 7,873 |
| Mtwara | 44,331 | 2,515 | 46,846 |
| Ruvuma | 7,456 | 13,799 | 21,255 |
| Iringa | 98,694 | 9,931 | 108,625 |
| Mbeya | 291,624 | 16,794 | 308,418 |
| Singida | 18,936 | 14,652 | 33,588 |
| Tabora | 76,607 | 5,756 | 82,363 |
| Rukwa | 54,182 | 4,034 | 58,216 |
| Kigoma | 27,799 | 2,709 | 30,508 |
| Shinyanga | 877,589 | 19,199 | 896,788 |
| Kagera | 79,391 | 8,456 | 87,847 |
| Mwanza | 269,818 | 14,793 | 284,611 |
| Mara | 1,006,535 | 22,543 | 1,029,078 |
| Manyara | 64,926 | 12,033 | 76,959 |
| Njombe | 20,707 | 3,897 | 24,604 |
| Katavi | 226 | 2,311 | 2,537 |
| Simiyu | 1,525 | 5,306 | 6,831 |
| Geita | 832,929 | 4,139 | 837,068 |
| **Jumla** | **7,857,681** | **362,881** | **8,220,562** |